TABIA YA KIKRISTO

Tabia ya Kikristo: Mpango wa Masomo

Maelezo mafupi -

SOMO LA KWANZA (#1):

I. Utangulizi kwa Tabia ya Kikristo.

II. Utumishi.

SOMO LA PILI (#2):

III. Unyenyekevu (majifunzo juu ya maisha ya Musa).

SOMO LA TATU (#3):

IV. Uongozi (mafunzo juu ya maisha ya Nehemia).

SOMO LA NNE (#4):

IV. Uongozi (inaendelea).
Nyongeza juu ya tabia ya uongozi kutoka kwa Nehemia.

V. Tabia ya kutokujistahi (maisha ya Francis wa Assisi).

SOMO LA TANO (#5):

VI. Malezi (maisha ya John Wesley). Mtihani.

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -

Tabia ya Kikristo: Mtihani

Maulizo inayowezekana kwa kuleta alama 20

1) Eleza tofauti katikati ya kuwa mtumishi na kutumika tu (uk. 6-8).
2) Zungumza juu ya hoja mbili muhimu ya asili ya unyenyekevu (uk. 11-13).
3) Zungumza juu ya unyenyekevu dhahiri ya jinsi gani Musa alitoa macho kwake yeye mwenyewe (uk. 18-19).
4) Zungumza juu ya njia tatu ambazo Nehemia kiongozi aliamsha watu wake (uk. 29-31).
5) Zungumza juu ya jinsi gani Nehemia kiongozi alisimamia na alijibu kwa ushindani (uk. 31, 32).
6) Fasiri jinsi uhuru na furaha ilikuwa matokeo ya maisha ya kutokujistahi iliongozwa na Francis wa Assisi (uk. 36,37).

Maulizo inayowezekana kwa kuleta alama 10

1) Toa habari kwa kifupi ya malezi ya "kutawadha ya miguu" (uk. 4).
2) Onyesha jinsi gani makatazo ya kutenda aina ya kazi ziliyo "nyenyekevu" ni ibada ya sanamu (uk. 5-6).
3) Unyenyekevu ya uwongo ni nini (uk. 10, 11)?
4) Jinsi gani maombi na unyenyekevu zina funga manisha (uk. 13)?
5) Kwa kifupi eleza maneno ya historia ya kitabu cha Nehemia (uk. 22).
6) Onyesha jinsi gani Nehemia alikuwa na matumaini ya asili/imani kwa Mungu (uk. 23).
7) Fasiri jinsi gani Nehemia aliepuka tatizo ya kukosa usawa katikati ya mamlaka na usimamizi (uk. 28).
8) Fasiri njia ya Nehemia ya kuamsha wengine (uk. 29).
9) Onyesha njia moja ambayo Nehemia aliongoza kwa njia ya kujitoa (uk. 33).
10) Taja moja ya tabia za Nehemia (tazama nyongeza) na toa marejeo (uk. 35).
11) Eleza wazi kabisa wazo ya kutokujistahi (uk. 36).
12) Toa fasiri mfupi ya tofauti katikati ya malezi na halali (uk. 39).

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -

I. Utangulizi Kwa Tabia Ya Kikristo.

A. Tabia: Kweli (hakika) ya Wewe ni Nani na Unafanya Nini.

1. Tabia ni neno yenye inatambuka maneno kama "nafsi ya mtu" na "umbo ama tendo la kuonekana." Tabia ni kile ulicho kabisa ni uhakika ya yenye kuwa nyuma ya umbo ama tendo la kuonekana. Ni uhakika ya yenye kuwa mbele ya nafsi ya mtu.

2. Ilinenwa:

   Wazo lako la ukamilifu ni kile ulitamani uwe.
   Sifa ama heshima yako ni kile watu wanasema yupo.
   Tabia yako ni kile yupo hakika.

3. Tabia yetu inaunda mwendeleo ya maisha yetu. Imenenwa pia:

   Kama tukipanda wazo, tutavuna tendo.
   Kama tukipanda tendo, tutavuna zoezi.
   Kama tukipanda zoezi, tutavuna tabia.
   Kama tukipanda tabia, tutavuna ajali.

B. Yaliyomo Katika Somo Hii.

1. Somo hii inajifunza mamoja ya hali ya muhimu kuliko kuhusu tabia ya kikristo. Kupitia mafunzo hii, tutaona wazi zaidi mkristo ni nani na mkristo anafanya nini.

2. Tabia katika alama zifuatazo zitafunzwa:

   a. Utumishi (kupitia mafunzo ya Yesu na wanafunzi).

   b. Unyenyekevu (kupitia mafunzo ya Musa).

   c. Uongozi (kupitia mafunzo ya Nehemia).

   d. Kutokujistahi (kupitia mafunzo ya Francis wa Assisi).

   e. Malezi (kupitia mafunzo ya John Wesley).

Maelezo mafupi -

II. Utumishi.

A. Yesu alitia kawaidi (kanuni) kwa utimishi wa Kikristo katika kuosha miguu ya wanafunzi ndani ya Yoane sura ya 13.

1. Malezi (utamaduni) kufuatana na nchi za Persia jinsi inavyo onekana katika Yoane sura ya 13: Kuosha miguu ilikuwa mazoezi kwa watu wote wa nchi za Persia hadi wakati wa Abramu (Mwanzo 18:4; 19:2).

   a. Ukavu wa nchi katika Upande ule ulifanya njia kuwa na uchafu wa namna yote na vumbi tele. Watu walivaa viatu ya wazi (makubazi) wakati walienda safari. Kwa hivyo, kuosha miguu ilikuwa mazoezi katika utumishi.

   b. Kuosha miguu ilikuwa namna ya utumishi wa chini kabisa katika utamaduni ya Waebrania.

      1) Wayaudi (Waebrania) hawa kuwa hata kuruhusu watumishi wao wenyewe wafanye kazi. Waliita mtumwa wao wa chini kabisa yule mtu wa mataifa ili aoshe miguu ya wageni.

      2) Kutosha tu wakati mwanafunzi aliosha miguu ya mwalimu kwa kuonyesha uaminifu wake kwa huyu (mwalimu).

2. Jinsi gani Yesu alitia kanuni mpya kwa utumishi wa Kikristo?

   a. Katika Yn 13, Yesu aliyekuwa mwalimu, aliosha miguu ya wanafunzi wake. Ujumbe ni wazi.

      1) Munanitumikia kwa kuwa mimi ni kiysongozi (mstari wa 13).

      2) Badala, ninawatumikia (mstari wa 14a).

      3) Kwa sababu, lazima mujitahidi kutumikiana (mstari 14b, 15).

         a) Inabidi tujitahidi kutumikia wengine kwa sababu yule anayekuwa mkuu kuliko sisi alijitayarisha kwa kutoa maisha yake kututumikia sisi.

         b) Kwa kusema wazi, wakati tunajilinganisha na Yesu na tunafi kiliza kwamba hali yetu inahusiana na yake, hatutajaribu kusema kwamba tuna haki fulani na kwa hiyo hatuwezi kufanya namna fulani ya kazi.

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi –

(1) Wakati tuankataa kufanya kazi kwa sababu ni "nyonge" zaidi, tunajitia wenyewe juu ya Yesu huyu aliyefanya kazi nyonge kuliko katika siku zake hapa ulimwengu. Tukifanya hivyo ni kama vile tunafanya ibada ya sanamu.

(2) Wakati Yesu alifanya kazi nyonge kuliko ilikuwa mfano aliyotupatia kwa kujishusha, hili kiburi chetu kisiwezi kutuzuia kufanya kazi lolote kwa kusaidia wengine, hata kazi hili ni "nyonge" kiasi gani.

Mfano ya Mwandishi:

Haibidi wachungaji waseme hawawezi kufanya kazi nyonge katika kanisa kwa sababu wana malezi ya Biblia.

Kwa namna hiyo pia haibidi wakristo wafanya kazi wakatae kusafisha choo za kanisa kwa sababu wanaona kwamba ni kazi yo chini zaidi kwa utumishi wao.

Tia mfano wako ndani:

Maelezo mafupi -

Kusudi la Mazungumzo

Sasa utumie kielelezo ifuatayo kwa kujadilia na kutumia wazo hii



Kumbuka kama wakati tendo ya utumishi iko chini yangu, ndipo nina weka Yesu chini yangu pia kwa sababu ninasema kama sinabudi kutenda ambayo alitenda. Hiyo inaniweka mime mwenyewe juu yake. Hii ni ibada ya sanamu.

B. Kuna tofauti katika ya mtu mwenye kutumika na mtu mwenye ni mtumishi.

1. Utumishi ya kweli na upendo ya kweli.

   a. Yesu kiisha kutoa habari wazi kwa wafuasi wake juu ya kutumikia (kurejezea iliyo juu), aliwaelezea kama watatumwa duniani na ye (Yn 13:16).

      1) Tunatumwa kuwa wafuasi wa Yesu. Sharti tugawe roho yake ya utumishi na kukubali njia ya maisha ambayo inafuatana na njia aliyochagua juu yake mwenyewe.

      2) Lazima tukumbuke kama Yesu akuandaa tu utumishi wa asili. Aligeuka Mtumishi wa kwanza.

      3) Hivyo, hatupashwe kufanya tu matendo ya utumishi. Lazima tuwe watumishi.

   b. Tunaweza kuona kama utimishi ya kweli ni tokea ya upendo ya kweli.

      1) Mtu mwenye kufanya matendo ya utumishi anaweza kuyafanya kutokana na nia zinazofichana . Mtu aliye mtumishi anafanya matendo ya utumishi kutokana na nia safi.

      2) Katika mfululizo ya MOTMOT juu ya Ndoa, namna mbili ya upendo zinapambanisha.

Maelezo mafupi –

a) Upendo wa "ulimwengu" umeitwa "hamsini kwa hamsini." Hii ni kusema kwamba kila mshiriki anajitoa nusu ama hamsini; anafanya yote nusunusu tu katika maisha ya ndoa. Kila mmoja anangojea mwenziye atoe sawa sawa mambo yote.

b) "Agape" upendo ni upendo halisi ama "mia juu ya mia." Hii ni kusema kwamba kila mshirika anajitoa mzima, ama anatoa maisha yake juu ya mwenziye mia juu ya mia katika ndoa yao. Kila mshirika anatamani kumsaidia mwenziye bila kungoja amrudishie upendo ule, ata kama utoaji hii ni ya kutumainia malipo, ao ni ya garama.

c) Mfano mmoja wa namna hii ya upendo. Utumishi "hamsini kwa hamsini" na utumishi "mia juu ya mia."

(1) Utumishi "hamsini kwa hamsini" ni ya kujifikiri mwenyewe (ya choyo) na ya uwongo.

(2) Utumishi "mia juu ya mia" ni halisi, ya upendo , ya kweli na yenyi haitumainie malipo.

Kusudi la Mazungumzo

Utumie kielelezo ifuatayo kwa kujadilia wazo iliyotangulia:

Namna Ya Utumishi	Yenye Inasema	Fafanusi
Utumishi isiyo halisi 50_____50 Alama ya utoaji	Nitakutendea kama unatenda. Nitafanya nusu (nitatenda kama utanirudishia)	*Katika elimu hii, hakuna utumishi wa kweli. Macho yako yanamtezamia mwengine. Utatenda tu kama wanakutendea kwanza. Mtu mwengine anangojea wewe utende kwanza.*
Utumishi halisi 100_____100 Alama ya utoaji	Nitakutendea hata chochote kifanyike. Nitafanya yote kama inalazimishwa.	*Katika elimu hii, kuna utumishi wa kweli, wa uhuru na yenyi hakikisho wakati wote. Macho yako yanatezamia madaraka yako mwenyewe utumishi wako haimtezamie mtu mwengine.*

c. Kwa kuwa mtumishi lazima usahau mataka yako na ukumbuke mataka ya mwengine.

Maelezo mafupi -

1) Lazima pia ukumbuke Shuguli yako mwenyewe na usahau Shuguli mwengine.

2) Kwa masemi mengine, lazima maisha yako ya choyo isiwe hai, uishi kwa Mungu na kwa ajili ya wengine.

2. Kuchagua kuhudumia na kuchagua kuwa mtumishi.

a. Wakati tunachagua kuhudumia, mara kwa mara tunabaki na mzigo ya kusema, ni nani, wakati gani, sababu gani, nafasi gani, ama jinsi tutahudumia. Hii kweli inatia mipaka kwa huduma yetu na pia inatufanyiza tujisikie kama vile watu wanaotumikishwa na wengine.

b. Wakati tunachagua kuwa watumishi tunacha "haki" yetu na tunajiingiza kafika kazi kutumikia wengine. Hakuna tena mipaka kwa utumishi wetu katika Kristo na hatuwezi kujisikia kama vile tunatumikishwa tu na wengine kwa sababu tumekwisha kutia chini haki yetu (kwa hiyo, hakuna haki yet iliyobaki yenye inaweza kutendewa jeuri (kuhasibishwa)

1) Hali ya kuwa mtumishi misingi yake yatokea makusudi yenye kutakaswa na matokeo yake ni utumishi halisi katika Yesu Kristo.

2) Paulo alijieleza mwenyewe kama mtumwa wa Kristo (Warumi 1:1; Wafilipi 1:1, na vivi hivi). Yesu alisema kwamba yeyote anayetaka kuwa mkuu lazima awe mtumwa (Mat 20:27).

a) Mtumishi wa namna hii anatia chini (anaachilia) haki zake zote kama afanyavyo mtumwa.

b) Kuachilia haki na kushikilia haki hiyo ndiyo tofauti kati ya yule anayehudumia na yule anayekuwa mtumishi.

Kusudi la Mazungumzo

Tumia Wafilipi 2:6,7 kwa kujadilia wazo hili.

c. Yesu alitumia fumbo ya mtumishi yule aliyetoka shambani kiisha kufanya kazi na akaendelea tu kuhudumia nyumbani. Hii ni mfano wazi wazi (hakika) ya mafundisho haya (usome Luka 17:7-10).

Maelezo mafupi –

1) Katika fumbo, mtumwa hana haki hata moja. Hapate hata haki ama sifa wakati anafanya kazi yake, kwa kuwa anatimiza tu mapashwa yake kama inavyostahili. Yesu alisema lazima tuwe na hali ya namna hii kama watumishi.

Kusudi la Mazungumzo

Tumia kielelezo ifuatayo kwa kuzidisha mazumgumzo kuhusu wazo iliyotangulia:

Hali Ya Utumishi Ya Kidunia			Hali Ya Utumishi Katika Ufalme wa Mungu		
Kusumbua wengine	Hahudumie hasumbue	Kuhudumia wengine	Hahudumie hasumbue	Kuhudumia wengine	Neema Ya Mungu
|	|	|	|	|	|
Nafasi mbaya (malipizi)	Hasiye ngambo moja (hakuna zawadi/hakuna malipo	Nafasi nzuri (zawadi)	Nafasi mbaya (malipo)	Hasiye ngambo moja (hakuna zawadi/hakuna malipo)	Nafasi nzuri (zawadi)

2) Dunia inafundisha kwamba kutokuhudumia ni kutokuwa na ngambo moja. Katika ufalme wa Mungu, kukosa huduma matokeo yake ni malipo (dhambi ya upuuzi). Zaidi kuliko, katika ufalme wa Mungu, kuhudumia haitegemee ngambo moja. Ni lazimisho tunayochukuwa. Haina zawadi. Zawadi ni matokeo ya neema ya Mungu.

Kusudi la Mazungumzo

Tumia kielelezo ifuatayo kwa kuzidisha mazungumzo kuhusu mawazo zilizotangulia kufuatana na tofauti kati ya wale wanaochagua kufanya kazi na wale wanaochagua kuwa watumishi.

MFANYAKAZI	MTUMISHI
Nimtumikie nani --- si halisi	Nani --- (yeyote kama vile Mungu anaamuru)
Kutenda kazi gani --- si halisi	Nini --- (yoyote kama vile Mungu anaamuru)
Nafasi gani kutenda kazi --- si halisi	Wapi --- (popote kama vile Mungu anaamutu)
Sababu gani kutenda kazi --- si halisi	Sababu gani --- (sababu yoyote kama vile Mungu anaamuru)
Wakati gani kutenda kazi --- si halisi	Wakati gani --- (kila mara kama vile Mungu anaamuru)
Jinsi gani kutenda kazi --- si halisi	Jinsi gani --- (walakini kama vile Mungu anaamuru)
Kama kanuni hizi zinaharibishwa, kwa hiyo kazi inakwisha.	Hakuna hali yenye inaweza kuharibishwa na kuweza kukomesha uduma.
Mfanya kazi anafanya kazi kwa muda. Ni kitu kimoja anachofanya tu. Jambo ama kitu hicho kinaukomo wake na kinafikia mwisho pia.	Mtumishi anafanya kazi kwa kuwa yeye ni mtumishi. Ni kile ambacho alicho. Kile ulicho mwenyewe hakiwezi kufikia mwisho ama kukomehswa.

Maelezo mafupi -

III. Unyenyekevu.

A. Utangulizi kuhusu unyenyekevu.

1. Hotuba ya kwanza ya Yesu mbele ya watu (inayoitwa hotuba Mlimani) inatia mkazo zaidi juu ya tabia ya ndani ya watu wanaoishi katika ufalme. Si kwa bahati fulani kuona kwamba tabia ya kati ya kwanza katika hotuba hii inaelekea unyenyekevu (Mat. 5:3).

   a. Kwa masemi mengine, uweza kwa kutimiza sifa za heri kama vile Yesu ametia mkazo katika hotuba ya kwanza inafuatana na kipimo unachofikilizia tabia ya ndani hii ya kwanza.

   b. Unyenyekevu ni tabia ya ndani moja ya kikristo yenye kufungua milango kwa tabia zingine. Ni kanuni (sharti) kwa kujenga tabia ya ndani ya mtu wa Mungu.

2. Kwa kujifunza unyenyekevu, tutachungua maisha ya musa. Biblia inasema alikuwa mnyenyekevu zaidi ya watu wote juu ya uso wa ichi (Hesabu 12:3). Kwa hivyo, mafunzo ya maisha yake inatutolea ufupisho mzuri yenye kutusaidia tuelewe vema "unyenyekevu."

3. Mustari wa kuwonyesha hii inachukua nukta tatu kuu:

   a. Asili ya unyenyekevu.

   b. Njia kwa unyenyekevu.

   c. "Alama" za unyenyekevu.

B. Asili ya unyenyekevu.

1. Kwanza tutazame ile isiyo unyenyekevu (unyenyekevu wa uwongo).

   a. Mtu yeyote anayesoma Hesabu 12:3 anaweza kufikiriia kwamba ufafanusi juu ya unyenyekevu wa Musa inapita kipimo.

      1) Waandishi wengine wana eleza unyenyekevu wa Musa kama vile kitu alichotoamani kujulisha (kuarifu) wengine hili apate mwenyewe kujikinga na kiburi (majivuno).

Maelezo mafupi –

2) Wanafafanua unyenyekevu wake kama vile hali iletwayo kwa kutendewa mbele ya watu badala ya jibu kwa Mungu. Ni kitu kimoja alichojaribu kufikilia.

b. Fafanusi hii ni fafanusi ya unyenyekevu ya uwongo na haina mapatano na unyenyekevu tunayoona maishani mwa musa.

1) Jifunza Wakolosayi 2:18-23.

2) Unyenyekevu ya uwongo yenye kutofautishwa na ile yenye "kukomaa na ukomaa yenye kutoka kwa Mungu (mstari 19b)." Matokeo yake kwa kutokuwa na kadiri (kima) ya kuzuia tamaa ya mwili (mstari wa 23b)."

2. Sasa tutazame asili (hali) ya unyenyekevu wa kweli.

a. Unyenyekevu asili yake ni ufunguo tatu.

1) Unyenyekevu haitafute ukubwa. Inatazamia Mungu.

a) Ingine namna ya kusema hii ni kwamba hii ni unyenyekevu isiyo ya kugombana kwa kuongoza, inafanya yote iongozwe na Mungu.

b) Maisha ya Musa ilikuwa maisha iliyojazwa na matendo yale Mungu alimwambia afanye. Ilikuwa maisha ya kuongozwa.

(1) Tunaona ata Musa aliongozwa mpaka kifo chake (Kumbukumbu 32:48-52).

(2) Soma kumbukumbu 34 uone jinsi gani Musa alifuata maelekezo haya.

2) Unyenyekevu inamtoa mtu toka binafsi yake mwenyewe katikati ya ukuu.

a) Mara kwa mara shabaa letu ni kwetu sisi wenyewe wakati tunazungumza juu ya ushindi wetu na kufanikiwa kwetu, lakini unyenyekevu inatuelekeza kwa Mungu.

b) Musa, kama hivyo watu wa Mungu wengi wanyenyekevu, alielekezwa kwa Mungu katikati ya ukuu wake.

Maelezo mafupi -

(1) Tazama maneno ya Yusufu katika Mwanzo 41:16 na pia maneno ya Danieli katika Danieli 2:27-30.

(2) Musa aliepuka jaribu ya kujipa mwenyewe sifa juu ya ushindi. Angalia jinsi gani katika kutoka 18:8, musa anamwelekea Bwana Yesu wakati anamwelezea Yetro kuhusu kutoka.

c) Mafundisho hii inashika pia wazo ya kwamba unyenyekevu si hali ya choyo yenye kujifaidia mwenyewe sababu ya bahati njema ama heri.

(1) Kwa mfano, katika bahati njema ya Musa, alipewa nafasi ya kuwa "kiyongozi mkuu wa taifa na mwenye maarifa." Walakini, alishugulikia zaidi heshima ya Mungu kati ya mataifa hayo yaliyosikia juu ya sifa njema yako" (angalia Hesabu 14:12-17).

(2) Tena tazama jinsi gani Danieli hakutafuta kujifaidia kufuatana na sifa njema yake (Danieli 5:17).

d) Asili ama hali ya unyenyekevu inaongoza watu watazamie sifa njema ya Mungu, ustahi, sifa nzuri, na utukufu badala ya kutazamia mambo ya kujifaidia wao wenyewe.

3) Unyenyekevu halisi, matukio yake ni kutokujali hata umuhimu wako mwenyewe.

a) Kama vile Yoana mbatizaji (Yoane 1:21) na Paulo (1 Tim 1:15), Musa hakujali hata juu ya kimo chake. Kumbuka jinsi gani Musa hakufambua kwamba uso wake ulikuwa ukingara kiisha kusimama mbele ya Mungu (Kufoka 34:29).

b) Lazima tutamke kwa nguvu kwamba unyenyekevu si ukosefu wa ustahi ama wa matumaini. Unyenyekevu inaelekeza kwa "ustahi ukuu wa Mungu" na "matumaini kwa Mungu," badala ya "kujisifu zaidi" na "kujitetea."

(1) Matumaini ya aina hii inatoka kufuatana na tumaini na ufungamano kwa Mungu. Ustahi inatoka kufuatana na utiifu kwake na ufahamu ya kuwa yeye ni Nani.

Maelezo mafupi –

(2) Kumbuka kwamba kujiona mtu bure, unyenyekevu wa uwongo ni onyesho ya kiburi. Wakati mwingine inaonekana kama unyenyekevu, lakini kwa keli ni jibu la kiburi lenye kulenga juu ya mtu binafsi ama mwenyewe. Kujiona mtu bure inasema "siwezi kufanya hicho" haya mara kwa mara ni matokeo ya kiburi ya mtu mwenyewe kujifikiria badala ya kumfikiria Mungu.

(a) Imeonekana kwamba ata mtu mnyenyekevu zaidi mbele ya uso wa ulimwengu alibidi kushinda aina hii ya unyenyekevu wa uwongo. Wakati Musa alijiona mtu bure alionyesha alama ya kiburi kwani alifikiria uwezo wake badala ya uwezo wa Mungu.

(b) Ona Kutoka Ex 4:10-14 na Kumbuka kwamba kwa sababu hii "Hasira ya Mungu iliwaka juu ya Musa."

b. Asili ya unyenyekevu pia inalinganisha pamoja Imani na maombi.

1) Imani.

a) Musa alikuwa mtu wa imani kwa sababu alielewa kwamba hakuweza kujisaidia mwenyewe na hakuweza kufanya lolote pasipo Mungu.

b) Imani inaanza na kuamini kweli inayopatikana katika Yoana 15:5. Unyenyekevu ndio chombo kitacho kuruhusu kuitika kweli hii.

c) Hivyo, kama vile kawida imani na unyenyekevu inalingana pamoja.

(1) Umbalimbali ya unyenyekevu kiburi) ni kukataa imani. Kwa kuwa imani yetu haituelekei tena wenyewe (kiburi), tunakibadilisha na imani yetu kwa Mungu, na tunaanza "kutembea kwa unyenyekevu na Mungu wetu"(Mika 6:8).

(2) Kwa kuwa mtu wa imani kuu, ni lazima kuanza kuwa mtu wa unyenyekevu zaidi. Musa alikuwa mtu wa imani kuu kwa sababu alikuwa mtu wa unyenyekevu sana.

Maelezo mafupi -

2) Maombi (sala).

a) Kuomba (kusali) ni kujinyenyekea mwenyewe mbele ya Mungu. Ni "vema" tumwambie Mungu," siwezi lakini wewe unaweza." Maombi (sala) inakuelekeza kuacha kujiangalia wenyewe na kumtumainia tu Mungu.

b) Hivyo si kitu cha mshangazo kuona kwamba mtu aliyekuwa mnyenyekevu kuliko ulimwenguni alikuwa pia muombaji mkuu. Musa alizungumza na Mungu bila kujitumainia, kwa uwazi, na unyenyekevu.

C. Kukua ya Unyenyekevu Katika Maisha ya Musa.

1. Mambo halisi namna yalivyo na mahali.

a. Miaka makumi mane (arobaini) katika kuamishwa inchini ya kigeni.

1) Mwanzo wa ukuzo wa Musa kama vile mtu mnyenyekevu ameanza na jambo yenye yalionyesha wazi kiburi kati yake.

a) Katika Kutoka 2:11-14 tunaona mtu aliyetaka kumtangulia Mungu na kuchagua mambo mikononi mwake mwenyewe. Ukosefu wa unyenyekevu wa Musa ndio ilimtuma ajaribu kuwakomboa wana wa Israeli katika utumwa wakati alimuuwa nu Midiani aliyekuwa akisimamia watumwa wayahudi. Kwa kufanya hivyo, alizarau wakati wa Mungu na utawala wake.

b) Kwa kinyume, Mungu alitumia tu ile ile maonyesho ya kiburi kwa kumsukuma Musa kuingia katika nafasi yenye ilibidi ajifunze unyenyekevu.

2) Kwa miaka arobaini (40) zilizofuata, Musa, mtu mkubwa wa Misri, aligeuka kuwa mchungaji mnyenyekevu wa kundi ya Yetro katika jangwa. Bila shaka, Mungu alitumia sehemu ya pili ya miaka arobaini ya maisha ya Musa, kwa kumfundisha unyenyekevu.

b. Mwito wa Mungu katika maisha ya Musa.

Maelezo mafupi –

1) Wakati Mungu alimwita Musa katika kutoka 3 na 4, tunaona matunda ya yale miako 40 ya kufundishwa unyenyekevu. Mbele yake mwenyewe, Musa hakuwa tena yule mtoto mume maalum aliyekuzwa katika jumba la mfalme Farao, yule aliyekuwa na uwezo wa kuwatoa wana wa Israeli toka utumwa wa maaduui zao. Alikuwa yule aliyenena, "Mimi ni nani?" wakati Mungu alimtuma awakomboe wana wa Israeli (Kutoka 3:10,11).

   a) Musa pia aliona wazi kukosa utoshelevu wake.

   b) Tazama wengine waliopokea mwito mkuu (Yeremia 1:6; 1 Samueli 9:21; Waamzi 6:15). Musa alielewa na aliona wazi tofauti kuu iliyokuwa kati ya kutokutosheka kwake kwa njia ya uweza wake mwenyewe na ujumbe aliyopewa.

2) Lazima tukumbuke wenyewe kwamba, kwa kipindi hiki maishani mwake, unyenyekevu wa Musa ililazimishwa ikomae (angalia fafanusi kuhusu kujiona bure).

   a) Haitoshe kwa unyenyekevu kusema, "siwezi kufanya hayo." Lazima unyenyekevu itimilize wazo hiyo na masema haya "Mungu anaweza."

   b) Musa hakuwa bado na unyenyekevu wa kutosheka kwa kutokujali udhaifu wake, kwa kutegemea nguvu za Mungu na utoshelevu wake. Hivyo, hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa (Kutoka 4:14).

UKUMBUSHO: Unyenyekevu wa Musa ilikomaa. Alijifunza kutegemea utoshelevu wa Mungu. Hivyo, badala ya Mungu kumwangalia Musa na hasira, akamwangalia na neema (angalia Kutoka 33:12-17).

c. Somo la unyenyekevu kwa Musa pale Refidi.

1) Ukomavu wa unyenyekevu wa Musa ilikuwa inalazimishwa papo hapo. Kiisha matendo makuu inayahusiana na miujiza katika Misri na wakati wa kuvuka bahari, Musa angeliweza kujehuriwa upesi kwa kiburi na kujitumainia.

2) Kwa namna ya kuvutia, Mungu alimtia Musa mbele ya jambo hapo Rifidi (Kutoka 17:1) hili aweze kumsukuma Musa kukumbuka ukosefu wa utoshelevu wake mwenyewe.

Maelezo mafupi -

a) Hakika, karibu ya kuuwawa kwake akipigwa mawe (Kutoka 17:4) Musa alikumbushwa juu ya hali ya kumtumainia Mungu kwa jumla. Alikua katika unyenyekevu jinsi aliona namna gani alimuhitaji Mungu zaidi.

b) F.B. Meyer ameandika, "Wakati tunafikilia mwisho wa nafsi yetu yenyewe, ndipo hapo tunafikilia mwanzo wa Mungu."[1]

2. Mwenendo kawaida ya unyenyekevu.

a. Wana wa Israeli wote walipitia mwenendo huu wa kuweza kujinyenyekea. Musa pia alikuwa mmoja wao.

1) Mungu aliwanyenyekeza wana wa Israeli (Kumbukumbu 8:3) na aliwajaribu (Kumbukumbu 8:16).

2) Kwa kawaida, mwenendo mzima wa kuzunguka jangwani na kutokuwa kabisa na msaada ilibidi hakika kuzaa unyenyekevu katka wana wa Israeli.

a) Wale walioonja miaka ya kuzunguka jangwani, walizoea mateso (taabu).

b) Wataalamu wengi wanafafanua (wanatafsiri) neno la kiebrania yenye inatafsiriwa kama "mnyenyekevu" katika Hesabu 12:3 kama vile imeshirikiana ama imelinganishwa na taabu. Waza ni kwamba taabu inazaa unyenyekevu.

b. Tunaposoma kupitia hesabu ya miaka arobaini ya mwisho ya maisha ya Musa tutaona jinsi gani hakuweza kujifaidia tena mwenyewe na hakutaka kufikiria mapashwa yake. Mingi na zaidi alifurahia mapenzi na mapashwa ya Mungu na kuwatumikia wana wa Israeli. Mwenendo hiyo Musa alipitia kwa kutokujifikiria tena mwenyewe na mapashwa yake ndio mwenendo hiyo hiyo alipitia pia kwa ukomavu wake katika unyenyekevu.

D. Alamo ya Unyenyekevu.

1. Utangulizi.

a. Katika sehemu hii tutatazama moja ya tabia (hali) na matendo yenye kuonyesha unyenyekevu.

b. Sehemu hii inaonyesha sura tatu kuu ya unyenyekevu.

1) Musa hakujitazamia mwenyewe.

2) Musa alitazamia wengine.

3) Musa aliheshimu wengine.

2. Musa hakujitazamia mwenyewe.

a. Ukosefu wa unyenyekevu inatuma mtu ajivune mwenyewe.

1) Watu wanajivuna kwa ajili ya maisha yao na kwa ajili ya yale waliotenda.

2) Watu wanajisifu kwa ajili ya ile wasiokuwa na kwa ajili ya hayo hawakufanya (ni ufahamivu wa uwongo kuhusu wao wenyewe).

3) Musa hakuanguka katika jaribu hii. Unyenyekevu wake ilimkinga hasiwezi kuuchukuwa utukufu kwake, wakati kwa wazi utukufu hii ilikuwa tu ya Mungu mwenyewe.

a) Kwa mfano, kiisha kuvuka bahari, Musa aliimba wimbo mzuri ya ushindi. Tunaweza kuuliza ulizo (swali): Nafasi gani kuna jina la Musa katika wimbo? Jibu ni kwamba haiko hapo (angalia Kutoka 15).

(1) Kuna marejeo 46 kwa Mungu katika wimbo ya Musa. Hakuna rejeo kwa Musa.

(2) Musa alikuwa na picha halisi (unyenyekevu) ya yeye peke yake. Alijifunza ya kwamba mtu ni chombo katika mikono ya Mungu. Chombo hicho inaweza kufanya kazi tu na ruhusa ya Mungu na musaada wake. Mafundisho hii inaendelezwa katika 1 Wakorinto 4:7.

b) Kwa wakati iliyoonekana kuwa rahisi kwa yeye kujitazamia, Musa hakujitazamia bali alimtegemea Mungu.

b. Matokio ya kukosa unyenyekevu ni kuchukua utukufu wa wewe mwenyewe.

Maelezo mafupi –

Maelezo mafupi -

1) Katika kutoka 34:34, 35, tunaona kama Musa angeliweza piga umalidadi uso wake wakungara kiisha kuwa mbele ya Mungu. Badala, aliufunika wakati alihitaji kusimulia na wengine.

   a) Unyenyekevu ulimuongoza hasiitike sifa.

   b) Unyenyekevu ulimuongoza kulumizwa kwa ajili ya wengine.

2) Tena, tunaona kama Musa hakujitezamia mwenyewe.

c. Ukosefu wa unyenyekevu inajaribu kukamata heri ya manufa yoyote kwa kufaidia mwenyewe.

   1) Musa alikuwa na manufa mingi kukamata heri yake ya sifa za watu, maongozi, na sifa njema. Labda angelijaribu kupata utawala ya mji mzima ya Misri (angalia Kutoka 11:3).

   2) Kitu cho chote chini zaidi ya unyenyekevu wa kweli ingeweza kumsukuma ajaribu kuchukua heri ya kikao. Musa, kwa vyo vyote, alitii maagizo ya Mungu na akuanguka kwa jaribu ya namna hii.

d. Ukosefu ya unyenyekevu inatokea kwa kuchukizwa wepesi na wengine.

   1) Musa aliisha katika mashtaki isiyo na haki siku zote. Hakutojali mashtaki hiyi, lakini unyenyekevu wake ilimkinga kwa kuchukizwa. Hakutafuta kulipiza kisasi juu ya washtaki wake.

      a) Angalia Kutoka 14:11-13; 16:2-8; na Hesebu 12:1-5.

      b) Musa, kama vile Kristo, aliacha utetesi yote ya lazima kwa Mungu. Alitukaniwa, lakini alibariki waliomtukana (tazama 1 Korinto 4:12).

   2) Wale walio wanyenyekevu hawahukumu wengine. Wanatumaini ya kwamba Mungu ni mwenye uwezo wa kuhukumu jambo barabara.

      a) Hivyo, unyenyekevu inahusiana sana na wazo la "raha" na amani. Unyenyekevu inawezesha mtu atowe cho chote kwa Mungu (pamoja na uchungu).

Maelezo mafupi –

b) Labda na wazo ilo moyoni, tunaweza kufahamu vema uhusiano katikati ya unyenyekevu na "kuweka wasiwasi yako yote juu yake (1 Petro 5:5-7)."

3. Musa alitazamia wengine, hapana yeye mwenyewe.

a. Ukosefu wa unyenyekevu inachagua kuitika sifa na heshima na haitowe uangalifu kwa wengine.

1) Katika Kutoka 32:10-12, Musa alitetea pamoja na Mungu kwa ajili ya wana wa Israeli, kwa hasara ya kupokea sifa kwa ajili ya yeye mwenyewe. Unyenyekevu wa Musa ilimruhusu kukana radhi yake mwenyewe na kutaka radhi ya wengine.

2) Angalia pia hali kama hii inayopatikana katika Hesabu 14:12-19.

b. Ukosefu wa unyenyekevu inataka kuchukua baraka zote. Haigawe.

1) Soma Hesabu 11:29 na Hesabu 12:1, 2.

a) Unyenyekevu inaleta tamaa ya kweli ya kugawa baraka. Unyenyekevu ni kitu amba cho kinamtuma mtu atamani kuona ushindi ya mtu mwengine.

Kusudi la Mazungumzo

Tazama nukta zilizotangulia kufuatana na mafundisho katika Wafilipi 2:3, 4.

b) Kiburi inazao nia kwa uficho yenye kutaka mwengine aanguke. Inaelekeza katika chuki na ukali wakati inaona uweza na majaliwa ya wengine.

Kusudi la Mazungumzo

Jadilie jinsi gani nukta iliyotangulia inahusiana na Warumi 12:3-6.

c. Ukosefu wa unyenyekevu haiwezi kutolea na kuzidisha uduma.

1) Unyenyekevu wa Musa ilimuruhusu atolee watu uduma bila kujaribu kuizuia kwake mwenyewe. Alileta uduma kwa furaha. Tazama hapa jinsi hakuna hata alama moja ya magomvi wakati alimwagiza Yosua katika Kumbukumbu 31:7 na Hes. 27:16-23.

Maelezo mafupi -

2) Kwa kuzidisha udhuma, lazima uwe tayari kuitoa kwa wengine. Musa alikuwa tayari kufanya hivyo. Tunalazima zaidi ya hali hii ya unyenyekevu katika kanisa siku hizi.

4. Musa aliheshimu wengine.

a. Ukosefu wa unyenyekevu matokeo yake ni kukosa kuheshimu wengine.

1) Unyenyekevu wa Musa ilimuwezesha aheshimu wengine.

2) Tazama masumulizi ya Musa na mkwe wake (Yetro).

a) Katika Kutoka 4:18, tunaona kwamba alitoka kupokea uongozi wa juu toka kwa Mungu mwenyewe. Hata hivyo, hakujiona mwenyewe kama wa muhimu kuliko hili awezi kukosa kuheshimu wazee wake. Musa na Yetro walifanya mapatano (Kutoka 2:21) an Musa alijinyenyekea kwa kuweza kuheshimu mapatano hayo hata angeliweza tu kuyazarau.

b) Katika Kutoka 18:17-27, tunaona kwamba Musa alikuwa kiyongozi wa kutoka ya miujiza. Alikuwa shujaha katika inchi ile yote. Hata hivyo, alizidi tu kupokea mashauri toka kwa Yetro, mwenye kwa wakati ule hakuonekana kuweza kutenda jambo lolote kuhusu wana wa Israeli.

c) Unyenyekevu ilimuwezesha Musa kumuheshimu Yetro. Heshima hii ilimuwezesha apokee na afadhili toka shauri yake.

b. Mara kwa mara ukosefu wa unyenyekevu inatuelekeza katika maisha ya kununguni ika

1) Musa hakuwa mtu wa kununguni kanungunika hata alikuwa na nafasi nyingi kwa yeye kuweza kunungunika. Unyenyekevu yake haikumruhusu anungunike.

a) Unyenyekevu inasema kwamba unaitikia kutokua na haki ya wewe kusimamia. Inasikilikana kwamba haustahili kitu chochote. Mungu analeta na anachukua jinsi atakavyo, kwa sababu yeye ni Mungu. Ana haki na uweza wa kufanya lolote atakayo. Mtu mnyenyekevu anaitikia hii. Matukio yake ni kwamba hanungunike.

Maelezo mafupi –

b) Unyenyekevu inaelekeza kupunguza mataka ya mtu kuhusu "Haki" yake. Majivuno inaelekeza kuongeza matumaini ya mtu kuhusu ile anayostahili. Kwa mwisho matendo haya Yanatuelekeza katika manunguniko.

2) Musa hakunungunika hata wakati hakuweza kuingia nchi iliyoagizwa.

a) Kama kuna mtu aliyekuwa na "haki" ya kudai chochote mbele ya Mungu ilikuwa Musa. Alitoa maisha yake mzima kuwaongoza wana wa Israeli katika nchi iliyoagizwa. Walakini, Mungu alikata kutokuacha Musa aingie nchi iliyoagizwa.

b) Musa hakunungunika. Unyenyekevu wake ilimuwezesha kuitika hukumu yake pasipo hata kutoa swali kwa Mungu. Hakuasi. Hakujaribu "kudai" haki zake. Hakutoa swali kwa usawa wa Mungu. Badala, alimtukuza Mungu (tazama Kumbukumbu 32:48-52; Kumbukumbu 33).

E. Mwisho.

1. Unyenyekevu ni sehemu ya lazima ya tabia ya Kikristo. Maisha ya Musa inatuandaa na mfano bora ya jinsi gani Mungu anaweza tengeneza sehemu hiyo ya tabia katika watu wake.

2. Inawezekana kwa kila mkristo kuomba unyenyekevu wa Musa iwe sehemu kawaida ya maisha yake ya maombi.

a. Ya kwamba sala sharti iweke ndani maombi kwa Mungu atupasishe na kiburi iliyo katika mawazo yetu, maneno, hali, na matendo.

b. Kama tunataka na tukiomba hiyo, ndipo Roho Mtakatifu ataanza kutumika maishani mwetu. Atatupasisha na kiburi, na kwa nguvu yake ataweka unyenyekevu badala ya kiburi.

IV. Uongozi.

A. Utangulizi.

1. Katika Kumbukumbu 28:13, Mungu alifanya ahadi kubwa sana kwa watu wake. Aliwaambia kama wakimtii, ndipo atawafanya kuwa "kichwa wala si mukia."

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -

a. Maisha ya wakristo katika ulimwengu iliyogeuzwa na kuanguka ya dhambi ya Adamu. Walakini, waliambiwa kwamba wanapashwa kuwa chumvi ya ulimwengu. Wanapashwa kuwa nuru (Matayo 5:13,14). Wanapashwa kuwa viongozi katika ulimwengu huu wa dhambi ili waongoze wafungwa wake walioanguka kwa uhuru.

b. Wakati wakristo si viongozi, ndipo ulimwengu inapatwa na matokeyo ya huzuni ya "kipofu akiongoza kipofu (Mat 15:14).”

2. Katika mfululizo hii kuhusu tabia ya Kikristo, ni lazima kujifunza umbo mbalimbali ya tabia ya kiongozi. Njia bora zaidi kwa kufanya haya ni kujifunza tabia ya Nehemia.

a. Kiweko cha kitabu cha Nehemia kinatafakari kandokando ya majengo ya taifa.

1) Katika mwaka wa 587 mbele ya kuzaliwa kwa Kristo, Wababiloni walisukuma Yuda kutoka inchi yao. Kiisha Babiloni kuanguka mikononi mwa Persia, mfalme kiro akapindua maongozi ya wababiloni iliyotangulia na akaruhusu wayahudi kurudi Yerusalema katika mwaka wa 538 mbele ya kuzaliwa kwa Kristo. Wayahudi wakwanza waliorudi Yerusalema walijenga madhababu na walijenga tena Hekalu (Ezra 1-6). Hata hivyo mji haikulindwa. Haikuwa na ukuta.

2) Katika mwaka wa 445 mbele ya kuzaliwa kwa Kristo, Nehemia akafika Yerusalemu kujenga tena ukuta za mji. Katika siku 52 nia kubwa ilitimizwa (Nehemia 6:15). Mungu alitumia Nehemia kuongoza wana wa Israeli watimize kazi kuu hii.

b. Hasa katika sura sita za kwanza, tunaona ustadi wa uongozi pasipo shaka ya Nehemia. Muhimu zaidi, tunaweza kujifunza sura hizi kwa kuanza kutunga mfano ya tabia ya kiongozi.

3. Majifunzo ifuatayo inatia jambo tatu kubwa ndani ya mstari yake:

a. Tabia ya kiongozi jinsi anahusiana na Mungu.

b. Tabia ya kiongozi jinsi anahusiana na wengine.

c. Tabia ya kiongozi jinsi anajihusu mwengine.

FAHAMU: Marejeo yote ya Biblia inahusiana na kitabu cha Nehemia isipokuwa ilionyeshwa kwa sababu nyingine.

Maelezo mafupi

B. Tabia ya Kiongozi jinsi Anahusiana na Mungu.

1. Kiongozi ana tegemeo halisi kwa Mungu.

   a. Jibu la kwanza la mara moja ya Nehemia juu ya kuwako kwa matatizo ilikuwa kumtafuta Mungu (angalia jinsi gani Nehemia alitenda haya katika 1:5).

   b. Nehemia mara moja alikumbuka Mungu wakati ililazimishwa kukata shauri (angalia jinsi gani Nehemia alitenda haya katika 2:4).

2. Kiongozi ni mtu wa maombi.

   a. Jinsi tulijifunza toka maisha ya Musa, tabia ya kiongozi inatiya tamaa ya kuongozwa na Mungu. Mtu anayeongozwa na Mungu sharti mara kwa mara angojee toka kwa Mungu.

      1) Nehemia alingoja na aliomba kwa miezi nne mbele ya yeye kutenda (mwezi wa Kisileu (1:1) kwa mwezi wa Nisani (2:1) ni ya kulinganika na mwezi wa Desemba kwa mwezi wa Aprili).

      2) Tabia ya kiongozi sharti imuwezeshe kudumu. Sharti angojee mara kwa mara kwa sababu Mungu si haraka kila mara kwa kutenda kama tulivyo!

   b. Kiongozi sharti atafute mpango wa Mungu badala ya kujaribu kufanya mpango wake mwenyewe. Hivyo, maombi yake si moja ambayo anaainisha katika akili na utashi yake mwenyewe. Mbele ya kuomba juu ya chochote dhahiri, anaomba kwanza apokee maongozi toka kwa Mungu kuhusu kuomba nini na kuamini kwa nini.

      1) Tunaweza kusema kwamba kiongozi anaomba maombi ya kutafuta mapenzi ya Mungu mbele ya kuomba maombi ya imani (ndipo imani yake inapata kitu kimoja kya kusimamia).

      2) Nehemia alipisha miezi nne kuomba maombi ya kutafuta mapenzi ya Mungu mbele aliomba maombi ya imani 1:11.

Maelezo mafupi -

c. Katika maombi, kiongozi hamuongozi Mungu zaidi kwa wale anayesimamia kadiri anavyoongoza wale anayesimamia kwa Mungu. Hamuambie Mungu kitu cha kufanya. Anawaonyesha wengine mbele ya Mungu, anaomba kwa ajili yao, na anamuomba, Mungu awasaidie na awaongoze.Anamuendea Mungu kwa ajili ya watu wake

1) Hapa lazima tuseme juu ya umuhimu wa wewe kujishirikisha ama kujifanya mumoja na watu anaoongoza. Ni kigumu kuenda mbele ya Mungu kwa ajili ya watu kama haujishirikishe na watu wale.

2) Kujishirikisha kwa maana ingine ni kama vile kuna "madaraka ya jamii (umoja)." Lazima kiongozi ajifanye mumoja na dhambi na uovu ya watu wake. Agano jipya inatuonyesha kwamba inabidi tupate mateso ama taabu pamoja (1 Wakorinto 12:26), muchukuliane mizigo yenu, na mulie (Bagalatia 6:2), na mulie (mutoe machozi) sababu ya zambi ya ndugu zenu (1 Kor 5:2).

a) Jifunza 1:6,7 kwa kuona jinsi gani Nehemia alimlilia Mungu kama vile mteteaji kwa ajili ya watu wake.

b) Virongozi wengine wakubwa kama vile Ibrahimu, Musa, Yeremia, na Danieli walifanya kilio ya maombi namna hii mbele ya Mungu.

(1) Wao wote walikuwa na wivu kuhusu heshima ya Mungu (kirongozi ni mwenye kuwa na uhusiano na Mungu).

(2) Wao wote walikuwa na upendo wa juu na wa kweli kwa ajili ya wengine (kirongozi ni mwenye kuwa na uhusiano na wengine).

(3) Wao wote hawakujali tu kuhusu maisha yao wenyewe. Hawakujifikiri wenyewe (kirongozi katika uhusiano na yeye mwenyewe).

3. Kiongozi ni mtu mwenye Imani.

a. Katika 1:5, tunaona kwamba Nehemia alikuwa mwenye kuwaza vema. Alikuwa mtu wa Imani. Msingi hii ya mafikira nzuri na Imani ilikuwa nini? Msingi yake ilikuwa juu ya vitu vitatu.

Maelezo mafupi –

1) Msingi hii ilishimikwa hatika kuamini kwake kwamba Mungu wake alikuwa na uweza wa kutimiza mahitaji yake. Mwanzo wa Imani ni wewe kujua Mungu ni nani. Ombi lake ilianza na matamko ya kusema Mungu ni nani, yenye ililenga juu ya uwezo wa Mungu, "eh Bwana Mungu wa mbingu, Mungu mkuu na mwenye kutisha.

2) Ilitegemezwa juu ya imani yake imara kwamba Mungu wake alikuwa mwaminifu na mwenye nia ya kujibu maombi yake. Imani inaendelea pamoja na wazo kwamba Mungu iko ngambo yako, si mbalimbali na wewe. Maombi yake iliendelea na ukumbusho kwamba Mungu ni Mungu wa usawa na mapendo "anayelinda maagano na wema."

3) Ilitegemezwa juu ya matumaini ya kuwa katika hali nzuri yeye mwenyewe. Imani inaleta ufahamu ya uko nani. Maombi ya Nehemia ilimalizika na mfano ya watu ambao Mungu alitamani kusaidia. Ni wale ambao walikuwa na uhusiano na Mungu na walimtii "kwa wale wanaompenda na kushika amri zake."

b. Tafsiri hii ya "fikira ya hakika" ni mbalimbali kidogo kuliko mafundisho ya kisasa ya kupendeza watu wote juu ya fikira ya hakika. Tafsiri ya Biblia inakaza juu ya maagizo ya Mungu na nini Mungu amekwisha nena. Mafundisho ya kisasa mara kwa mara inakaza juu ya tamaa za mtu na nini mtu ananena.

c. Kumbuka, imani inaweza kungojea kwa Mungu. Mafundisho ya kisasa kwa ajili ya imani mara kwa mara inatia mkazo kwa wazo la furaha ya ghafula. Kwa kuangalia hitaji ya maombi au ahadi toka kwa Mungu, mafundisho hii husema kwamba tunaweza "kuitaja na kuidai."

1) Mafundisho ya Biblia kuhusu imani mara kwa mara inatia mkazo kwa maana ya imani na utumishi (na mara kwa mara mateso) iliyo funikwa (soma katika Waebrania 11). Kwa kuangalia ahadi toka kwa Mungu, husema kwamba imetupasa "kuipokea na kuiamini."

2) Wakati wangojea, imani inaweza kuona yatakayokuja (mbele) pasipo kukana ukweli ya kisasa (hii inabishana na hali moja moja ya "maungamo ya asili" ya elimu ya imani ya watu wengi.

Maelezo mafupi -

4. Kiongozi umjua Mungu.

   a. Nehemia alikuwa mtu ambaye alimjua Mungu na ahadi zake (tazima 1:8,9). Tunaweza kuona jinsi gani mtu amjuaye Mungu, aliye kiongozi wa kweli, ataonyesha jinsi gani mtu yule anaweza kuongoza wengine.

Mafafanusi ya Mwandishi:

Mchungaji maalum wa nyuma katika mchezo wa miguu ya ki Amerika anajua jambo linalofikiri wasimamizi wa kikundi chake wanapokuwa nje ya kiwanja. Zaidi kuliko, ni kwa huyu mchungaji wa nyuma ndipo wachezaji wengine wanaangalia hili wapate maelekezo kwa mchezo kwa kuwa yeye kuliko wengine wote anasikia vema amri ama maonyo zinazotolewa na wasimamizi hapo nje ya kiwanja.

Tia Mafafanusi Yako:

   b. Katika njia ile ile, kiongozi mwema anajua sauti ya Mungu na njia zake

5. Kiongozi aogopa Mungu.

   a. Nehemia alitamani kukataa mazoeo ya viongozi wa nyakati yake (tazama 5:15).

      1) Mara kwa mara katao ya mazoeo inasukumwa kwa maasi juu ya amri, uchungu, au tamaa kwa kupata faida ya ifuatayo.

      2) Lakini, kusudi ya Nehemia ilikuwa safi. Alikataa mazoeo ya viongozi wa nyakati yake kwa sababu aliogopa Mungu.

         a) Alitamani kufurahisha Mungu tu. Hakutia fikira kwa kujifurahisa mwenyewe au watu wengine.

Maelezo mafupi

b) Hivyo, tendo lake "la awali" iligeuka tendo ya kawaida lenye kuwiana na tamaa ya Mungu (Warumi 12:2).

b. Kiongozi mwema sharti ajongelee Mungu.

1) Moyo wake wa ibada na juhudi kwa Mungu sharti isukume na ivute wengine kujongelea kwa Mungu.

2) Kweli hii ilitokea katika uongozi wa Nehemia kama vile alitia moyo kwa watu waliodhulumiwa kujaribu na kutimiza kazi iliyokuwa kama isiyowezekana.

C. Tabia ya Kiongozi Vile Anahusiana na Wengine.

1. Kiongozi wa nguvu anafahamu usimamizi na matengenezo.

a. Chanzo msingi ya usimamizi bora ni kuonyesha mahitaji ni nini mbele ya kuweka kiolezo.

1) Nehemia alifuata chanzo hii katika kutoa maswali kuu iliyokaza juu ya watu (1:2).

2) Kiongozi wa nguvu anakadirisha mahitaji, baadaye anajenga maarifa kufuatana na yale mahitaji.

Mfano wa Mwamdishi:

Mwendeshaji wa kikundi hafanyi maarifa bila kutazama kwanza nguvu na udhaifu wa wachezaji wake. Kwanza anakaidirisha uwezo ya wachezaji wake na kiisha anajenga (anatengeneza) maarifa kufuatana na haya.

Andika mfano wako:

Maelezo mafupi -

b. Mafundisho msingi ya matengeneo ni kuongoza watu kufuatana na vikundi vya watu wa jamii vinavyokuwa zamani ama miundo mbalimbali zisiyopunguzika.

1) Nehemia alifuata mafundisho hii na akatia watumishi wake katika matumizi kufuatana na watu wa jamii (3:1, 3), wa mjini (3:2, 13), na mafundi wa zahabu (3:8), watu wa uchumi (3:1, 28), kabila mbalimbali (3:17), na watawala wa nafasi mbalimbali (3:9, 12, 15-17).

2) Nehemia alionekana wazi kuwa bingwa wa matengeneo. Yapata vikundi makumi tatu na tisa mbalimbali vya wafanya kazi, vilitumika katika maatumio ya kujenga.

c. Sehemu muhimu kuhusu masimamizi ni kuwakilisha madaraka. Kiongozi asiyeweza kuwakilisha madaraka yake siye kiongozi hakika. Mwisho wake atawaharibu wale anaoongoza, kinyume chake ni kwamba ataharibu uongozi wake mwenyewe.

1) Viongozi watimilifu wanawakilisha madaraka na mamlaka kwa sababu wanaweza kuaminia wengine wapo salama katika vyeo vyao, katika uwezo na mamlaka. Kumbuka mafundisho ya Biblia toka Matai 16:25, kama unajaribu kulinda kitu ama kukiponyesha hatakipoteza.

2) Alama zingine za viongozi wa kweli zinaonekana katika namna ya kuchagua, katika malezi, na katika kuinua wengine kwa cheo. Orodha ya wafanyaakazi wa majengo katika sura ya tatu inafunua mapenzi ya Nehemia kutaka kuwakilisha uweza na madaraka.

d. Msimamizi mkamilifu anaepuka kukosa linganisho kati ya uwezo na madaraka.

1) Mtumishi anayepewa amri zaidi (hukumu) kuliko madaraka mwisho wake atavunjwa moyo na atachoka (atasumbuka).

2) Mtumishi anayepewa madaraka mingi kuliko uwezo ama amri ataangamizwa na atakosa ukamilifu.

a) Nehemia aliepuka kukosa linganisho. Kila mtu alipewa nafsi kamili ya ukuta na alikuwa na madaraka ya kuyajenga. Alipewa amri ama uwezo juu ya kazi pa nafasi ile (4:15).

Maelezo mafupi –

b) Matokeo yake ni kwamba wafanya majengo walikusudishwa zaidi katika ukamilifu kwa sababu walijua hakika yale waliotumainiwa kufanya (kutimiza).

2. Kiongozi mtimilifu ana uwezo wa kukusudisha wengine.

a. Kufa moyo inaweza kuwa adui mkuu zaidi wa kiongozi. Kama unaondosha kusudi kwa kufuata kikomo, ni kama vile unaongoza gari ama unakokota gari kubwa lenye magudurumu na mpira yenye kutoboka.

1) Kwa ngambo ya Nehemia, jambo la kushusha moyo iliwafikia watumishi kwa njia ya kupoteza nguvu, ufunuo na matumaini (4:10), na upotevu wa usalama (4:11).

2) Jinsi gani Nehemia alijibia kuhusu kuvunjwa moyo na adui?

a) Aliunganisha juhudi ya watu wake kwa kidomo ya watu wote (4:13).

b) Anongoza uangalifu wao kwa Bwana (4:14).

c) Alishika usawa wa uzito katikati ya mawazo na matendo (4:15,16).

d) Aliainisha na alieleza wazi jambo hili kila mtu apate nguvu (4:20).

e) Alitia moyo na alitengeneza njia kwa watu ili wasaidiane kila mtu na mwenziwe (4:21,22).

b. Kiongozi mtimilifu anaamsha wengine kwa kuweka mfano mwema.

1) Viongozi bora hawasukumi. Wanakokota kwa kuandaa mfano bora ya kufauta. Angalia 5:14-19.

a) Nehemia aliweka mfano wa huruma na kutolewa kwa haki zake (5:14, 15).

b) Aliweka mfano wa toleo (5:16).

c) Alitowa mfano wa kazi nguvu (4:23).

Maelezo mafupi -

2) Wakati mfano haifatiwe, kiongozi lazima awe tayari na aweze kutia nguvu kwa maadili inayofaa.

3) Nehemia alionekana kama mtu wa uwezo katika matengeneo kama vile tunasoma juu ya watu wa cheo wa tamaa (5:1-13).

c. Kiongozi mtimilifu anakusadisha kwa njia ya kujenga uhusiano thabiti ya kipekee.

1) Ufahamu wa Nehemia kuhusu majina ya viongozi wake, na kurudilia msemwa "akatengeneza sehemu nyingine" (3:11, 19-21, 24-27, 30), inafunua utambuzi wake mwenyewe kuhusu bidii ama juhudi ya watu wake wa kazi.

2) Kuju likana na kiongozi inaundda alama ya kijamii na hali ya usalama kati ya wafuasi (wanafunzi).

3) Sifa na utambuzi ni jambo mbili ya lazima kwa kukusudisha.

d. Kiongozi mtimilifu anajifunza jinsi gani kukusudisha na nia ya kati.

1) Makusudisho ya nje (feza, mapumziko) inakusudisha tu kwa muda kitambo ama kidogo.

2) Makusudisho ya ndani (ya kati) (kufurahika na kazi, maana ya azimio) inakusudisha siku zote.

a) Hakika, majifunzo mengi kuhusu uongozi wa uchumi inaonyesha thamani kubwa ya makusudisho ya kati na inaonyesha mipaka ya makusudisho ya nje.

b) Nehemia alitumia makusudisho ya ndani katika 2:17 wakati aliomba watumishi wajipe moyo hili kazi hii iwejuu ya sifa la Taifa.

Maelezo mafupi –

e. Mwenendo wa Makusudisho.

1) Kiongozi mtimilifu anaonyesha kazi jinsi inayofaa hili litimilizwe vizuri. Kiisha lazima aanzishe kazi katika matendo. Kwa mwisho, lazima aonyeshe kama kuna matumaini kwa hayo. Mwenendo hii inasogea toka uhakika, tendo, hadi imani.

2) Tumia kielelezo ifuatayo kwa kuonyesha jinsi Nehemia alitumia hii njia ya makusudisho (rejea katika 2:16,17).

MWENENDO WA MAKUSUDISHO

Onyesha kazi	Anzisha Tendo	Leta Tumaini
UHAKIKA	TENDO	IMANI
"Tazama"	"Jenga"	"Amini"

3. Kiongozi mtimilifu anafahamu jinsi ya kukomesha upingaji.

a. Kama kiongozi haukumiwe kwa mambo, inawezekana kwamba hafanyi kazi yake kama inavyostahili (tazama Luka 6:26).

b. Upingaji mara kwa mara inalingana na ushindi. Zaidi vile unapinganisha, zaidi hivyo utakuwa na ushindi kuliko. Lazima viongozi waweze kujibia na hekima kwa wapingaji wao.

c. Nehemia alijibia wapingaji awa kwa utimilifu katika 6:1-8.

1) Anatambua shina ya upingaji katika 6:12.

2) Kiisha anatambua kusudi ya upingaji katika 6:13.

3) Hakuruhusu matendo ya upingaji imufadhaishe yeye mwenyewe ama watu wake. Waliendelea, wakitia macho yao kwa ukomo wa kazi pahali pa kushugulika na upingaji. Walizidi kutia lengo lao juu ya ujumbe.

4) Alitumia maombi (4:4, 5, 9) na bidii (4:6) kwa kupiganisha upingaji. Alitumia pia akili ya kawaida (busura) (4:9).

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -

Mfano wa Mwandishi:

Kama unafikiri kwamba mtu mmoja anaweza kufungua gari yako akitaka kuiba, utaomba (utafanya sala) na utaamini kwamba Mungu atakinga gari yako. Pia utafunga milango ya gari (hii ni akili ya kawaida).

Andika Mfano Wako:

a) Nehemia hakuwa na Imani ya kutazamiwa ama ya kiburi. Alikuwa mtu wa maombi (sala) na matendo. Kumbuka jinsi gani inasemwa katika 4:9, "Tukaomba Mungu kuweka walinji."

b) Tendo haikanushe Imani. Tendo ni sehemu ya Imani.

D. Tabia ya Kati ama Sifa Njema ya Kiongozi Kuhusu Yeye Mwenyewe.

1. Kiongozi mkristo anaendelea kujitoa kwa ajili ya wengine.

   a. Kiongozi mkristo anakusudisha kufuatani na mahitaji ya wengine, hapana tu kwa mahitaji yake pekee. Lazima kiongozi awe "mwenye kuelekea kwa ajili ya wengine," hapana mwenye kujielekea mwenyewe. Lengo la kiongozi litakuwa juu ya matimilizo za wengine hapana juu ya matimilizo yake mwenyewe.

      1) Katika kutaja watu wake wa kazi na matimilizo zao, Nehemia hakutia lengo juu yake mwenyewe. Lengo lake lilikuwa juu ya matimilizo ya wengine.

      2) Kiongozi mkristo ni mwenye kuwa tayari kukaripiwa zaidi hata kuliko yale anayostahili, na pia yupo tayari kupokea tu sifa ndogo (heshima kidogo) kuliko yenye anayostahili kupata.

b. Lazima kiongozi mkristo awe na uwezo wa kuacha kujiangalilia (kujifikiria) mwenyewe hivyo apate kuwafikiria wengine. Kama anajisumbua sana na anahangaikia mambo yake mwenyewe, hivyo hataweza kusaidia wengine. Lazima awe huru (kutokana na yeye mwenyewe) hili apate kutumikia. Lazima awe huru hili awe na huruma juu ya wengine.

1) Yesu alikuwa na uwezo wa kusikilia vikundi vya watu huruma kwa sababu hakujitazamia yeye mwenyewe na mahitaji yake, lakini alifikiria wengine na mahitaji yao (tazama Mk 6:31-39).

2) Nehemia pia hakujifikiria mwenyewe, hivyo alisikia huruma juu ya wale aliongoza (angalia 1:4).

2. Kiongozi mkristo anonyesha kujitoa kwake.

a. Kiongozi mkristo anabidi kujitoa kwa ajili ya watu wake. "inabidi ajitolee" kwa ajili ya wale anaoongoza.

1) Kufuatana na Biblia, mume ndiye kichwa (kiongozi) wa mke (Waefeso 5:23). Madaraka yake kama vile kichwa (kiongozi) inatolewa kwa ufupi katika Waefeso 5:25. Anapashwa "kujitolea kwa ajili yake."

2) Kama kiongozi hana haki kwa njia hii, basi hayupo tayari kuongoza watu wake kwa utimilifu. Kama hayupo tayari kutoa maisha yake kwa ajili ya wale anaoongoza, hatimaye ndipo atapoteza kusudi lake kwani hakika amepoteza maana ya kusudi ama nia yake.

a) Bila wazo thabiti na ya maana, bila nia isiyo fairiwa vema, ni kugumu kuwa kiongozi. Nia hilo inalazimishwa kuelekea zaidi baraka ya wale wanaoongozwa.

b) Viongozi hawawezi kujiacha wenyewe wazuiwe na mapambano ya faida. Hawawezi kuachia faida yao na matakwa (tamaa) yao njia nafasi ya kutia mbele kwanza faida na mahitaji ya watu.

b. Lazima viongozi wakristo wawe tayari kwa kujitoa na ustahi (na heshima) kufuatana na maisha yao.

Maelezo mafupi -

1) Inabidi wakatoke kuishi katika utajiri wingi wa mali (anasa) wakati wale wanaoongozwa wanaendelea kuishi katika umaskini.

2) Hii nukta ni yale muhimu, pengine kuliko sababu zingine zote, kwa sababu inaonyesha ukweli ama uaminifu wa kiongozi (angalia 5:14, 17, 18).

Kusudi la Mazungumzo

Jadilie jinsi gani matendo ya Nehemia ilionyesha ukweli na uaminifu wake.

3. Viongozi wakristo wanaonyesha unyenyekevu.

   a. Viongozi wakristo sharti wajitezamie wenyewe kwa njia ya unyenyekevu. Hawawezi kuwa na hali ya kudharau au ya kiburi juu ya wao wenyewe. Unyenyekevu ingelitoka kwa uwezo wa kutumika pamoja na watu.

      1) Katika 2:17, Nehemia alijitia mwenyewe pamoja na watu.

         a) Hakusema:"Hii ni hoja lako. Hii ndiyo unalazimishwa kufanya"

         b) Anasema: Hii ni hoja letu. Hii ndiyo tunalazimishwa kifanya."

      2) Katika 4:23, Nehemia akatumia maneno haya kufanya kazi.

         a) Alitumika pamoja na watu wake. Alisimama kando kando yao na mikono yake ilipata uchafu pia.

         b) Hakuwa wa kujivuna kwa kutumika nguvu sana. Alikuwa mnyenyekevu wa kutosha kwa kutumika kazi nyonge jinsi aliongoza watu wanyonge.

   b. Viongozi wakristo wamewekwa msalabani.

      1) Kiongozi mkristo lazima ajifanye mwenyewe mumoja na Kristo, ambaye alijifanya mwenyewe mumoja na msalaba. Ni kwa njia hii tu ndipo ushindi wa ufufuo inaingia katika maisha na uduma ya kiongozi.

      2) Umbo hii ya kiongozi, zaidi kuliko njia ingine yote, imefanyizwa katika uhusiano wa ndani na wa nguvu pamoja na Mungu.

3) Tunaweza kusema kwamba kiongozi bora anaweza kuwa na nguvu ya kutenda vema wakati yupo kitukinachovuta. Wlakini, kiongozi mkuu ni mwenye nguvu ya kutenda vema wakati yupo yeye mwenyewe tu. Viongozi wakuu wamewekwa kwa wakati wao wanapisha pamoja na Mungu.

Maelezo mafupi –

E. Nyongeza ya Hali na Tabia ya Ndani ya Uongozi Toka kwa Nehemia.

1. Imani (4:14, 15, 20; 6:16).
2. Maombi ama sala (1:4-11; 2:4; 4:4, 5, 9; 5:19; 6:9,14).
3. Mwepesi kwa kuona (2:12).
4. Kumcha Mungu (5:9, 15).
5. Anamtegamia Mungu (2:8, 18).
6. Mwenye elimu, hekima na maarifa (1:2; 2:8, 12-15).
7. Busara (6:12).
8. Mwenye tendo la kuelekea(2:17).
9. Kwa kazi (3:21-23, 28-30).
10. Udumu (4:21).
11. Uteuzi (2:12-16).
12. Unyofu (5:9-12, 14-19).
13. Matengenezo (2:6-8, 11-16).
14. Uhodari (6:11).
15. Ya Busara (2:5-8).
16. Hasira la adili (5:6).
17. Mwenye kukinga njia ya uharibifu (4:13).

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -

V. Tabia ya Kutokujistahi.

A. Utanjulizi kwa Kutokujistahi

1. Labda tunaweza daribia zaidi tafsiri kwa neno moja ya tabia ya Kikristo ni yale ya kuwa "asiyejistahi."

   a. Kutokujistahi ni sehemu ya tabia ya mtu yule anauwezo ya kusahau matakwa na tamaa zake mwenyewe ili akumbuke matakwa na tamaa za wengine.

   b. Kutokujistahi ni tabia inayomruhusu Kristo kuishi ndani yetu. "Wala si mimi mwenye kuhishi (kutokujistahi), lakini Kristo ni hai ndani yangu (Wagalatia 2:20)."

2. Kwa kifupi, tutaangalia mumoja ya tabia ya maisha ya Francis wa Assisi, mfano toka historia ya kanisa ambaye aliishi karibu na mwaka 1200 wa nyakati zetu, ili tupate kusikia zaidi kabisa wazo la kutokujistahi katika tabia ya mkristo. Hase, mifano mingi bora ya historia ya viongozi wa kanisa (sawa vile Martin Luther, na vivi hivi) yangeweza chaguliwa.

Kusudi la Mazungumzo

Francis wa Assisi aliongoza maisha ya kutokujistahi. Tamaa yake kuu zaidi ilikuwa kujisahau mwenyewe kwa mwigo ya maisha ya Kristo. Maisha yake ilikuwa yenye kuamchwa kwa sababu alikubali kwa moyo roho iliyoongoza Kristo kwa msalaba (Matai 16:25). Alikubali kwa moyo roho ya kutokiyistahi. Katika njia gani unaweza kufuata kutokujistahi?

B. Uhuru na Kutokujistahi.

1. Uhuru kwa kutokujistahi na kania vile utumwa kwa kujipendeza. Kujipendeza inatuweka watumwa wa sisi wenyewe. Kutokujistahi inatuweka huru kwa sisi wenyewe na huru kumtumikia Mungu na wengine.

2. Francis wa Assisi alipata uhuru katika kutokujistahi kwake.

   a) Siku moja, alikuwa akiangalia uhuru wa ndege. Aliifuata juu ya nyumba. Alitembea polepole kwa mpaka ambako ndege alikuwa akisimama. Hapo ndege akaruka. Ndege ilikuwahuru.

Maelezo mafupi –

b) Francis alitamani kuruka pia. Alitamani kuwa huru. Alitambua kwamba kwa kuruka alipashwa kuwa mweupe. Alipashwa kujiweka huru mwenyewe na mzigo ya uzito aliyekuwa akibeba. Alipashwa kujifia ama kujisahau mwenyewe.

c) Angalia maana ya Matai Mt 11:28-30 kufuatana na maelezo ya uhuru.

3. Uhuru ilimtuma Kristo msalabani. Kuna uhuru katika kutokujistahi na "Pahali roho ya Bwana anapokuwa, kule kuna uhuru (2 Kor 3:17)."

Kusudi la Mazungumzo

Jadilie maana ya Wagalatia 5:13 na 1 Petro 2:16 jinsi inahusiana na wazo hizi juu ya uhuru na kutokujistahi.

C. Furaha na Kutokujistahi.

1. Furaha ni matokeo ya kutokujistahi. Huzuni ni matokeo ya kujiangalia (kujifikiri).

   a. Francis alieleza wafuasi wake kwamba ni madaraka yao wenyewe kujazwa na furaha na kuinua mioyo ya wengine.

   b. Francis alikuwa mtu wa furaha kwa sababu kutokujistahi kwake ilikuwa ya hakika. Hakujilazimisha mwenyewe kwa kujifia mwenyewe. Alikufa kwa kutaka kwa sababu alitamani kuwa kama Kristo. Hivyo, mateso na maadili yake ilifanyizwa katika furaha.

2. Kutokujistahi ya kweli inaonekana kwa roho ya furaha.

   a. Francis alipenda kufunga ama kutokula. Haikuwa mzigo kwake. Hakupendezwa nayo kwa sababu alikuwa masochist (mtu mwenye kupenda kujiadhibu mwenyewe). Alipendezwa nayo kwa sababu nia zake kwa kufunga zilikuwa kweli.

   b. Roho ya dini au ya kujifikiri inaongoza kwa huzuni. Roho ya kweli au ya kutojistahi inaongoza kwa furaha.

Kusudi la Mazungumzo

Jadilie jinsi gani hii ni kweli katika maneno yafuatayo:
Matai 13:44; 2 Kor 8:2; Wafilipi 2:17,18.

Maelezo mafupi -

FAHAMU: Zifuatazo ni maneno iliyosemewa na Francis kuhusu kutokujifikiria.

D. Masemi toka Francis wa Assisi.

1. "Juu ya neema zote na vipawa vya Roho Mtakatifu yenye Kristo alileta kwa kanisa, neema kuu zaidi ni ushindi juu ya kujifikiria mwenyewe, na kwa moyo mwema kwa ajili ya upendo wa Kristo kuvumilia maumivu na matusi na haya na ukosefu" (Luka 6:22, 23)."[2]

2. Kwa marejea ya hekima, urahisi, umaskini, unyenyekevu, upendo, na utii kama vile uadilifu, Francis anasema: "Kwa kuwa inatoka kwa Bwana, uadilifu takatifu zaidi yenye unaendelesha mbele. Na hakuma mumoja kati yena anayeweza kuyatumia bila kujikataa mwenyewe."[3]

VI. Malezi.

A. Utangulizi kwa Malezi.

1. Kwa kujifunza tabia ya Kikristo, inabidi pia tutazame wazo kuhusu malezi. Maisha ya Kikristo inabidi kawa maisha ya malezi. Malezi hii inabidi kukusudishwa na upendo wa Kristo.

2. Neno mfuasi (mwanafunzi) inatoka kwa shina la neno ile ile iliyounda neno malezi. Mkristo mwanafunzi ni yule anayemfuata Yesu Kristo na anaongoza maisha yake kufuatana na mfano wa Yesu.

3. John Wesley, mwanzishi wa mwendo ya wa Methodist, alikuwa mtu wa malezi. Alikuwa mtu wa taratibu (ndipo hapo jina la Methodist linatoka) katika kutembea yake pamoja na Mungu.

   a. Lakini hakuwa mtumwa wa sheria. Ukristo wake haikuwa kitu alichojifunyia kwa nguvu yake mwenyewe.

   b. Alikuwa hakika mkristu aliyejitoa sana. Ukristu wake (na malezi yenye iliendelea pamoja) ilikuwa kitu chenye alifanya kwa uhuru na furaha.

   c. Malezi yake ilikuwa ya muhimu kuliko chochote, njia ya kulenga na kutengeneza nguvu zinazojaa mwilini, kujipa mwenyewe ama kujitoa, na nia nzuri alikuwa nayo kwa ajili ya Kristo.

Maelezo mafupi –

4. Tutatumia maisha ya Wesley kua kujifunza kwa ufupi jinsi gani malezi ni hali ya muhimu katika tabia ya mkristo. Mifano mingi nzuri toka hadisi ya kanisa ingeliweza kuchaguliwa (kama vile mfano wa John Calvin).

B. Shirika Takatifu.

1. Mwanzo katika maisha ya Wesley, aliongoza kikundi kilichoitwa "shirika takatifu" Shirika ili lilitenda malezi mengine pamoja.

   a. Walifanya maombi ya kufunga mara mbili kua juma.

   b. Walikuwa na wakati wa sifa, maombi, na majifunzo ya Biblia pamoja toka saa kumi na moja ya asubui mpaka saa tatu ya asubui kila siku.

   c. Waliomba kwa ajili ya wamaskini toka saa kumi na mbili ya jioni mpaka saa moja ya jioni kila siku.

   d. Walisoma vitabu vya ibada na elimu ya dini pamoja toka saa moja ya jioni mpaka saa tatu ya jioni usiku tano kila juma.

2. Washiriki wa shirika takatifu walikuwa na maadili. Walakini hawakuwa na maadili ya bure bure tu katika maisha yao. Maadili yao iliamshwa na mapendo kwa Mungu na tamaa yao ya bidii nyingi kwa kumjua.

C. Uhuru si Kujifanya Watumwa wa Sheria (siyo utumwa wa sheria).

1. Maadili iliyotengenezwa kwa mwanzo ya Methodist inaweza kuonekana kwa wengine sawa inakaribiana na kujifanya watumwa wa sheria.

   a. Lakini, chama cha Methodist haikutia msingi kwa maadili ya uwezo wa mtu, lakini juu ya upuziko wa Roho Mtakatifu na tamaa kwa urafiki wa sana pamoja na Mungu.

      1) Maadili ilifanyizwa kwa sababu ya tamaa ya utakatifu. Haikuwa mwisho. Ilikuwa tu njia kwa kufika mwisho, ambayo ilikuwa kumjua Mungu zaidi.

      2) Mkazo wa maadili haikuwasukuma watu kufanya kitu kimoja. Ilikuwa juu ya kualika watu katika uhusiano thabiti na ya kufaa sana pamoja na Kristo.

Maelezo mafupi -

b. Maadili ya kusukumwa inaweza kuongoza kwa kujifanya mtumwa wa sheria. Lakini, maadili inayotokea kwa upumziko wa ROHO na shauri la kutaka ya mtu mwenyewe itaongoza kwa uhuru wa maisha.

2. Malezi haiko sababu ya wokovu. Ni matokeo.

a. Ni jibu kwa Mungu kusema kwamba, "Nataka kukutolea maisha yangu yote kwa sababu ulinipa maisha yako yote." Malezi ni yenye inaweza na inastahili kutumiwa kwa (kutimiza) "kufanyiza wokova wako" (Wafilipi 2:12).

b. Hivyo, malezi inashirikiana zaidi na utakatifu kuliko jinsi inayokuwa na wokovu. Jinsi tunavyotii kazi ama tendo la Roho kwa kututakasa, tutakuwa watiifu ama wasikivu zaidi na zaidi kwa ngambo mbali mbali ya maisha yetu.

c. Lengo la Malezi katika tabia ya Kikristo ilibidi kuwa juu ya utakaso (utakatifie) na uhusiano pamoja na Mungu.

1) Lazima mkristo awe mtiifu hili aweze kutia mwili wake chini ya uchunguzi wake (1 Kor 6:12-20).

2) Malezi hii lazima iwe zaidi kuliko "malezi ya mwili tu." Lazima itimizwe katika njia ya kumcha Mungu (1 Tim 4:7, 8).

3) Zaidi kuliko vyote, tabia ya Kikristo yenye kushikilia malezi ilibidi kuelekea zaidi kuhusu kupitisha muda pamoja na Mungu. Lazima tutiishe akili yetu (fikira) kwa kuzidi kukaa ama kudumu mbele ya uso la Mungu. Ilibidi tujizoeze sisi wenyewe kupanga na kuishi kufuatana na daftari yenye itatia mbele za yote kwanza kuketi muda ama kudumu pamoja na Mungu.

Kusudi la Mazungumzo

Mzungumze kuhusu jinsi gani Wakristo wa mbelembele (wa mwanzo) walionyesha malezi katika tabia zao. Mzungumze juu ya maana halisi na mashindano mbali mbali kama hivyo inaonekana katika Matendo 2:42.

Tabia ya Kikristo: Muhtasari wa Mwisho

Maelezo mafupi -

[1]F.B. Meyer, Musa (Fort Washington, PA: Christian Literature Crusade, 1978), uk. 101.

[2]D.K. Chesterton, Mtakatifu Francis wa Assisi (Garden City, N.Y.: Image Books, 1957).

[3]Sawa na iliyo juu.

TABIA YA KIKRISTO

Maelezo mafupi -